**HOTUBA YA MHE. KASSIM MAJALIWA MAJALIWA (MB), WAZIRI MKUU WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA KWENYE MAADHIMISHO YA SIKU YA UKIMWI DUNIANI MKOANI KILIMANJARO, TAREHE 01 DISEMBA, 2020**

**SALAMU**

- Mheshimiwa Anna Mghwira, Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro;

- Bibi. Dorothy Mwaluko, Katibu Mkuu - Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera na Uratibu);

- Profesa Mabula Mchembe, Katibu Mkuu, Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto;

- Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais – TAMISEMI;

- Makatibu Wakuu wa Wizara zote mliopo hapa;

- Viongozi na Watendaji Wakuu wa Serikali mliopo hapa;

- Mheshimiwa Zlatan Milisic, Mwakilishi Mkazi wa Umoja wa Mataifa Nchini Tanzania;

- Mheshimiwa Dkt. Donald Wright, Balozi wa Marekani Nchini Tanzania;

- Dkt. Leonard Maboko, Mkurugenzi Mtendaji wa Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania;

- Waheshimiwa Wabunge mliopo hapa;

- Viongozi wa Vyama vya Siasa mliopo hapa;

- Bibi Leticia Mourice, Mwenyekiti wa Baraza la Watu Wanaoishi na Virusi vya UKIMWI;

- Wadau wa Maendeleo mliopo hapa;

- Viongozi wa Madhehebu ya Dini mliopo hapa;

- Wageni Waalikwa;

- Wanahabari;

- Mabibi na Mabwana.

**Habari za Asubuhi.**

## SHUKRANI

**Ndugu Wananchi; kwanza kabisa,** nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema, kwa kutujalia afya njema na kutuwezesha kujumuika pamoja siku hii ya leo kwa ajili ya kuadhimisha Siku ya UKIMWI Duniani kwa mwaka huu wa 2020.

**Aidha**, nitumie fursa hii kuwashukuru na kuwapongeza wenyeji wetu mkiongozwa na Mheshimiwa Anna Mghwira, Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro kwa maandalizi mazuri ambayo yamekuwa chachu ya kufana kwa maadhimisho haya ya kitaifa ambayo kwa mwaka huu yanafanyika mkoani Kilimanjaro. **Hongereni sana!**

**Vilevile,** natoa pongezi nyingi kwa Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania (TACAIDS), iliyopo chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu, kwa kuendelea kuratibu vema maadhimisho haya mwaka hadi mwaka sambamba na kurahisisha upatikanaji wa elimu na huduma mbalimbali kwa wananchi na wadau wengine.

**Ndugu wananchi,** kama mnavyofahamu, tukio hili la leo ni moja ya shughuli zangu za mwanzo kuzitekeleza tangu Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aniteue kuendelea kumsaidia majukumu ya Uwaziri Mkuu kwa kipindi cha pili cha uongozi wa Awamu ya Tano.

Hivyo, kabla sijaendelea na hotuba yangu, naomba mpokee salamu za pongezi kutoka kwa Mheshimiwa Rais wetu mpendwa pamoja na Mheshimiwa Mama yetu Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais. Viongozi wetu hao, wanatupongeza sana kwa kufanikisha maadhimisho haya ya kitaifa ya Siku ya UKIMWI Duniani kwa mwaka 2020.

## MAADHIMISHO YA SIKU YA UKIMWI DUNIANI

**Ndugu Wananchi,** licha ya janga hili la UKIMWI kugundulika mwanzoni mwa miaka ya themanini hadi sasa tayari limegharimu maisha ya takriban watu milioni 35 ulimwenguni huku wengine wapatao milioni 38 wakiishi na Virusi vya UKIMWI (VVU). Hali hii inaufanya UKIMWI kuwa miongoni mwa majanga makubwa kabisa kuwahi kutokea katika historia ya dunia.

Hivi sasa, sote tunashuhudia maendeleo makubwa katika kukabiliana na janga hili yakihusisha kutungwa kwa sheria dhidi ya unyanyapaa kwa watu wenye kuishi na VVU sanjari na kuongezeka kwa uelewa wetu kuhusu janga hili.

Hata hivyo, licha ya juhudi na hatua mbalimbali zinazochukuliwa katika kujikinga na maambukizo ya VVU bado namna ya kujikinga na kuwakinga wengine pamoja na unyanyapaa vimeendelea kuwa ni changamoto katika Jamii zinazotuzunguka.

Kwa msingi huo, Siku ya UKIMWI duniani inabaki kuwa ni muhimu kwa kuwa inaikumbusha Serikali na Umma kuwa UKIMWI bado upo. Kadhalika, bado tunahitaji kuendelea kukusanya fedha, kuongeza uelewa wa watu wetu kuhusu janga hili na kupambana na vitendo vya unyanyapaa. Kwa lugha nyingine, Siku ya UKIMWI Duniani imebeba malengo yafuatayo:

**Mosi**: Kuwakumbuka maelfu ya wenzetu waliopoteza maisha kutokana na UKIMWI;

**Pili**: Kuwakumbuka na kuwajali maelfu ya watoto yatima ambao wazazi wao walifariki kutokana na UKIMWI; na

**Tatu**: Kuwatia moyo Watu wanaoishi na VVU na wale wote wanaowahudumia;

**Ndugu wananchi**, jambo la msingi zaidi ni kwamba, hii ni siku ambayo Taifa na wananchi wote kwa pamoja tunatafakari upya tulikotoka, tulipo na tunakoelekea hususan katika harakati zetu za kupambana na UKIMWI. Ni dhahiri kuwa tutafanikiwa katika vita hii kwa kuweka mikakati mipya na endelevu.

Lengo ni kuhakikisha yale malengo ya SIFURI TATU ifikapo mwaka 2030 ambayo ni kudhibiti maambukizi mapya ya VVU yasitokee, kukomesha unyanyapaa na kutokomeza vifo vitokanavyo na UKIMWI yanafikiwa kwa wakati.

**KAULIMBIU YA SIKU YA UKIMWI DUNIANI MWAKA 2020**

**Ndugu Wananchi**, baada ya kuwasili kwenye eneo hili, nilipata fursa ya kutembelea baadhi ya mabanda ya maonesho. Kupitia mabanda hayo, nimejionea utoaji wa huduma za elimu, uhamasishaji na upimaji wa Virusi Vya UKIMWI (VVU) na magonjwa mengine yasioambukiza.

Nikiri tu kwamba nimevutiwa na mambo mengi ikiwemo huduma zinazotolewa na wadau mbalimbali kwenye mabanda hayo ya maonesho. Hivyo, natoa pongezi na shukrani kwa wadau wote mliojumuika katika utoaji wa huduma na elimu kwa wananchi katika wiki yote hii iliyoanza tarehe 25 Novemba 2020.

Napenda kuwahakikishia kwamba Serikali inathamini na kutambua yale yote mnayofanya katika mapambano dhidi ya VVU na UKIMWI nchini.

**Ndugu Wananchi,** jambo lingine lililonivutia kwenye maadhimisho haya ya mwaka huu ni Kaulimbiu ya Maadhimisho ya mwaka huu wa 2020 inayosema **"Mshikamano wa Kimataifa, Tuwajibike Kwa Pamoja"** yaani ***Global Solidarity, Shared Responsibility***.

Kama inavyojidhihirisha, kaulimbiu hii inahimiza suala zima la kuimarisha UMOJA NA USHIRIKIANO katika jitihada zetu za kupambana na VVU na UKIMWI. Kwa kufanya hivyo, tutakuwa kwenye nafasi nzuri ya kuhakikisha kuwa tunaimarisha Afua za kinga dhidi ya maambukizi mapya ya VVU pamoja na mifumo ya kiafya.

**Ndugu wananchi**, kwa kuimarisha umoja na ushirikiano tutamudu kuhakikisha kuwa Afua za kiafya zinapewa rasilimali za kutosha; upatikanaji wa dawa za kutosha za kuokoa maisha; kuendeleza tafiti za kutafuta chanjo dhidi ya VVU na UKIMWI; kuheshimu haki za kibinadamu na kuzingatia haki za wanawake na mabinti pamoja na usawa wa kijinsia.

**Ndugu wananchi**, kwa upande mwingine kaulimbiu hii inalenga kuhamasisha mataifa, wananchi, makampuni, taasisi na makundi mbalimbali ya jamii na watu binafsi **kushikamana, kuwajibika na kushiriki kikamilifu** kwenye shughuli za kudhibiti VVU na UKIMWI duniani na nchini.

**Ndugu Wananchi**, iwapo tutaimarisha mshikamano na uwajibikaji, kwa pamoja tutaweza kufikia lengo la kuwa na Dunia na Tanzania isiyo na maambukizi mapya ya VVU ifikapo mwaka 2030.

## MWENENDO WA MAPAMBANO DHIDI YA VVU NA UKIMWI

**Ndugu Wananchi,** kuadhimishwa kwa Siku ya UKIMWI Duniani leo hii mkoani Kilimanjaro ni sehemu ya utaratibu tuliyojiwekea kuwa tutakuwa tukiadhimisha siku hii kila mwaka katika mikoa mbalimbali ya nchi yetu. Kadhalika, niendelee kusisitiza kwa wasimamizi wa maonesho haya kuhakikisha yanafanyika kote nchini katika ngazi ya mikoa, Halmashauri na hata Vijiji. Aidha, kila mkoa uliowahi kufanya maadhimisho haya uhakikishe kuwa unawasilisha taarifa yake Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania ndani ya mwezi mmoja kuanzia leo.

**Ndugu Wananchi,** Vijana ni kundi linalokabiliwa sana na changamoto ya maambukizi mapya ya VVU nchini. Takwimu za maambukizi mapya ya VVU zinaonesha kwamba asilimia 40 ya maambukizi hutokea kwa vijana na katika hao asilimia 80 ni vijana wa kike.

Kwa mujibu wa takwimu hizi, ni dhahiri kuwa kundi la vijana na hasa wa kike lipo kwenye hatari kubwa zaidi ya kupata maambukizi mapya. Uchambuzi wa kimazingira kuhusu takwimu hizi unaonesha kuwa sababu za vijana kuwa katika hatari ya maambukizi mapya ya VVU ni pamoja na zifuatazo:

**Moja**: Kuanza ngono katika umri mdogo. Hali hii husababisha mhusika kuwa na mahusiano ya mapenzi na watu wengi hadi anapofikia utu uzima. Hivyo, kujiweka katika hatari ya kupata maambukizi ya VVU. Nawaasa vijana, msijihusishe na mapenzi katika umri mdogo. Ili vijana muweze kutimiza ndoto au malengo yenu katika Maisha; lazima kuwa na Subira;

**Mbili***:* Vijana wadogo wa kike kuwa na mahusiano ya kingono na wanaume wenye umri mkubwa kwa kuvutika na vishawishi kama vile pesa na zawadi ndogo ndogo. Kwa mara nyingine tena, natoa rai kwa wanaume wenye umri mkubwa kuachana na tabia ya kujihusisha na mapenzi na wasichana wadogo. Niwakumbushe tena, Serikali haitasita kuchukua hatua kali za kisheria kwa yeyote atakayebainika;

**Tatu**: Matumizi yasiyo sahihi na endelevu ya mipira ya kike na kiume. Takwimu zinaonesha kuwa vijana wengi wanaojihusisha na mapenzi hawatumii kinga na wengine hutumia mara moja tu na baada ya kuzoeana huendelea na mahusiano ya ngono bila kinga yoyote;

**Nne**: Ulevi wa kupindukia na matumizi ya dawa za kulevya hususan kuchangia sindano wakati wa kujidunga huchochea vijana kuambukizwa VVU kirahisi; na

**Tano**: Unyanyasaji wa kijinsia na ukatili dhidi ya watoto unaombatana na matendo ya ubakaji, udhalilishaji na vipigo. Vitendo hivi, vimekuwa chanzo cha kuongezeka kwa watoto wa mitaani. Pia, huchochea kushamiri kwa maambukizi mapya ya VVU.

**Ndugu Wananchi**, hizo ni baadhi ya sababu au vichocheo vya kuongezeka kwa maambukizo mapya ya VVU miongoni mwa vijana.

Aidha, natoa wito kwa vijana kujitambua na kuthamini maisha yao kwa kujikinga na maambukizi mapya ya VVU kwa kuwa ninyi ni nguvu kazi na Taifa linawategemea. Na wale wanaoishi na VVU waendelee kutumia dawa za ARV kwa ufuasi sahihi bila kuacha ili kufubaza VVU na kuimarisha afya zao.

## MAFANIKIO KATIKA MAPAMBANO

**Ndugu Wananchi,** katika mapambano dhidi ya VVU na UKIMWI, nchi yetu imepata mafanikio makubwa. Mafanikio hayo ni pamoja na;

Kupungua kwa kiwango cha watu wanaoishi na Virusi vya UKIMWI (yaani WAVIU) kutoka asilimia 7.0 (mwaka 2004) hadi kufikia asilimia 4.7 (mwaka 2017).

Aidha, maambukizi mapya kwa mwaka nayo yamezidi kupungua kutoka watu 130,000 mwaka 2001 hadi 68,484 mwaka 2019. Pia, vifo vitokanavyo na UKIMWI kwa mwaka vimepungua kutoka vifo vya watu 85,000 mwaka 2001 hadi kufikia vifo 21,529 mwaka 2019.

**Ndugu wananchi,** pia nimearifiwa hapa kuwa nchi yetu imefanikiwa kufikia malengo hayo ya TISINI TATU (90:90:90) hasa katika 90 ya pili na ya tatu. Kwa kujikumbusha tu ni kwamba TISINI TATU zinalenga kuhakikisha kuwa asilimia 90 ya WAVIU wanajua hali zao; asilimia 90 ya wanaojua hali zao wanaanza kutumia dawa za kufubaza mapema na asilimia 90 ya walioanza dawa za kufubaza VVU kinga zao za mwili zinaimarika kufikia 2023.

Natoa wito kwa wadau wote katika mapambano dhidi ya VVU na UKIMWI, tuongeze jitihada sana katika kuhamasisha upimaji wa VVU ili tufikie lengo katika 90 ya kwanza pia.

Vilevile, tuendelee kujitathmini katika maeneo yote matatu ili palipo na changamoto tuweze kurekebisha na kuimarisha na penye mafanikio tuongeze nguvu zaidi badala ya kubweteka. Aidha, mipango yetu ya baadaye ioneshe wazi jinsi tutakavyofikia Tanzania isiyokuwa na UKIMWI ifikapo mwaka 2030.

**Ndugu wananchi,** Mafanikio yote haya yametokana na kuendelea kuimarika kwa huduma za tiba ikiwemo matumizi ya dawa za kufubaza VVU (ARV) na Afua za kinga zinazohusisha tohara ya kitabibu kwa wanaume na kuzuia maambukizo ya VVU kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto. Serikali pamoja na wadau wetu wote tutaendelea kuhakikisha tunaimarisha upatikanaji na ubora wa huduma kwa wananchi wote na kufanya tafiti zitakazopima matokeo ya juhudi zetu ili kujipanga zaidi kimkakati ili kutokomeza janga hili ifikapo 2030.

## MIKAKATI YA KUENDELEZA MAPAMBANO NA KUDHIBITI MAAMBUKIZI

**Ndugu wananchi,** pamoja na mafanikio makubwa tuliyoyapata, bado kuna mambo mengi yanayohitaji kufanyika ili tuweze kufikia adhima yetu ya kumaliza kabisa janga la UKIMWI. Hii ni pamoja na kuzuia maambukizi mapya sambamba na kuzuia vifo vinavyotokana na UKIMWI na hatimaye tuanze kuona gharama za kudhibiti VVU na UKIMWI nchini zikipungua.

**Uwekezaji bunifu katika mapambano:**

Gharama zikipungua, rasilimali fedha hiyo itatumika kufanya uwekezaji kwenye maeneo mengine ya maendeleo nchini. Ninaamini kuwa, uwekezaji unaoratibiwa vema kwenye kudhibiti VVU na UKIMWI utawezesha kupunguza kasi ya kuenea kwa VVU, kupunguza madhara kwa WAVIU na watu wengine kwa mtu mmoja mmoja, familia na jamii kwa ujumla.

Natoa agizo kwa TACAIDS, Wizara ya Afya na wadau wote wa kudhibiti VVU na UKIMWI nchini, tujipange vizuri kubaini na kufanyia kazi maeneo mbalimbali ya uwekezaji katika kudhibiti VVU/UKIMWI yenye gharama nafuu lakini yatakayoleta matokeo makubwa.

**Kuimarisha njia za mapambano kwa vijana;**

**Ndugu Wananchi,** naelewa kuwa kutokana na kasi ya maambukizi mapya ya VVU kwa vijana kuwa juu, maadhimisho haya kwa miaka mitatu mfululizo yamekuwa yakiweka mkazo katika maonesho na huduma rafiki kwa vijana katika KIJIJI CHA VIJANA. Napenda kusisitiza kuwa kampeni za mawasiliano ya mabadiliko ya tabia kwa vijana ni lazima ziwe endelevu kupitia njia mbalimbali zikiwemo vyombo vya habari na mitandao ya kijamii.

Lakini pia, kama nilivyotoa maelekezo miaka mitatu iliyopita, kwa mara nyingine naielekeza Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania (TACAIDS) iendelee kufanya kazi na majukwaa ya wasanii ili kuwafikia vijana wengi zaidi. Halikadhalika, Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto nanyi hakikisheni huduma-rafiki za ARV nchini zinapatikana kwa wanaozihitaji na muendelee kutoa elimu kuhusu umuhimu wa matumizi bora na endelevu ya dawa hizo.

**Kuimarisha huduma kwa watu wenye ulemavu:**

**Ndugu wananchi,** katika kufikia Tanzania isiyokuwa na UKIMWI ifikapo 2030, tusisahau kundi la walemavu. Watu wenye ulemavu mara nyingi hukosa fursa ya kusema mahitaji yao maalum au kusikilizwa kutokana na hali na nafasi zao kwenye jamii. Kama walivyo wananchi wengine, watu wenye ulemavu wanahitaji huduma ya elimu ya VVU na UKIMWI, upimaji na matibabu pamoja na huduma za afya ya uzazi kwa upana wake.

Natoa wito kwa taasisi zote zinazoshughulikia masuala ya watu wenye ulemavu kuhakikisha Jamii ya watu wenye Ulemavu inashirikishwa ipasavyo kwenye mipango na mikakati ya kutoa hamasa na elimu hapa nchini. Watu wenye ulemavu ni lazima wajumuishwe kikamilifu kwenye mwitikio wa taifa dhidi ya VVU na UKIMWI.

**Kuimarisha huduma kwa watu wazee:**

**Ndugu wananchi,** ni vema wote tukatambua kuwa UKIMWI hauna jinsia wala umri kwani wapo watu wenye umri wa kuanzia miaka 50 na kuendelea ambao wanaishi na VVU na hivyo kuhitaji muda mrefu wa huduma za VVU na UKIMWI. Huduma za upimaji na matibabu nazo zinapaswa kuzingatia mahitaji ya kundi hili pia.

Wale wanaokutwa na maambukizi ya VVU hawanabudi kuingizwa kwenye mfumo wa matibabu kwa haraka, kwa sababu kinga za mwili kwa kundi hili huathirika haraka zaidi kulinganisha na vijana na hivyo kuhitaji muda mrefu wa kupatiwa huduma. Hivyo nasisitiza kuwa rasilimali na mipango izingatie uwepo wa kundi la wazee.

Aidha, huduma za UKIMWI kwa kundi la wazee ziende sambamba na huduma za magonjwa yasiyoambukiza kama vile shinikizo la damu, kisukari na magonjwa ya moyo. Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto hakikisheni mnaweka utaratibu bora wa huduma za VVU kwa ajili ya kundi hili. Watoa huduma kwenye kundi la wazee kuanzia umri wa miaka 50 wanatakiwa kupewa mafunzo ya namna bora ya kutoa huduma ikiwa ni pamoja na huduma za kisaikolojia na matibabu stahiki.

**Kudhibiti unyanyapaa:**

**Ndugu Wananchi,** sote tunafahamu kwamba unyanyapaa umekuwa ni kikwazo kikubwa katika kutekeleza mipango tuliyojiwekea wenyewe katika kutokomeza UKIMWI. Serikali kwa upande wake, imeendelea kuchukua hatua mbalimbali ikiwa ni pamoja na kufanya kampeni za kuelimisha kuhusu madhara ya unyanyapaa na ubaguzi kupitia vyombo vya habari na majukwaa mbalimbali. Hata sasa kuna kampeni zinaendelea kupitia wasanii, mitandao ya kijamii pamoja na hotuba za viongozi.

Naomba mfahamu kuwa baadhi ya mambo yanayorudisha nyuma juhudi za udhibiti wa UKIMWI ni unyanyapaa na ubaguzi. Huu ni mtazamo potofu dhidi ya wengine wanaodhaniwa kuwa ni tofauti katika jamii. Mtazamo huu hufifisha upatikanaji wa haki kwa baadhi ya watu kwa kuonekana kuwa hawastahili na hivyo kutengwa.

Unyanyapaa huchochea uoga wa kupima VVU kwa hiari na kupata unasihi na huduma za ARV kwa wale wanaobainika kuwa

na VVU. Kwa mujibu wa takwimu za utafiti wa viashiria vya UKIMWI (Tanzania HIV Impact Survey -THIS 2016/2017), unyanyapaa na ubaguzi uko kwa kiwango cha asilimia 25 kwa watu wenye umri wa miaka 15-49 na asilimia 31 kwa wenye umri wa miaka 50 na umeshamiri zaidi maeneo ya vijijini.

Nawasihi Watanzania wenzangu, tuache kabisa tabia za unyanyapaa na ubaguzi. Elimu iendelee kutolewa kwa njia mbalimbali kuanzia ngazi ya familia ili watu wajue ukweli kuhusu VVU/UKIMWI pamoja na kujua jinsi ya kuwahudumia watu wanaoishi na VVU ili kuondoa mtazamo hasi.

Niwasihi Viongozi wa Dini zote, Wanasiasa wote na Viongozi wa Serikali katika ngazi zote, endeleeni kusemea na kukemea unyanyapaa na ubaguzi dhidi ya WAVIU na kuhimiza upendo na huruma miongoni mwao.

## MCHANGO WA WADAU KATIKA MAPAMBANO

**Ndugu wananchi**, katika kufikia mafanikio hayo niliyokwisha yataja, hatukuwa peke yetu. Wapo wadau mbalimbali ambao wamekuwa begabega na Serikali katika kuhakikisha tunashinda vita hivi dhidi ya VVU na UKIMWI. Hivyo basi, nitumie fursa hii kutoa shukrani za dhati kwa Mfuko wa Dunia (Global Fund).

Mfuko huu, ndiyo umekuwa mfadhili mkuu wa mradi wa Wasichana waliopevuka na mabinti (Adolescent Girls and Young Women - AGYW) kwenye mikoa ya Dodoma, Singida na Morogoro. Mradi huo, umeweza kuwafikia wasichana 21,871 (16,011 walio shuleni na 5,860 walio nje ya shule).

Vilevile, ninaishukuru Serikali ya Marekani kupitia Mfuko wa Rais wa Marekani wa Kupambana na Kudhibiti Maambukizo ya UKIMWI (PEPFAR) kwa kufadhili mradi wa DREAMS. Mradi huo, unalenga Wasichana waliopevuka na Mabinti walio nje ya mfumo rasmi wa shule wapatao 100,000 katika Mikoa ya Dar es Salaam, Mbeya na Shinyanga.

**MFUKO WA UDHAMINI WA KUDHIBITI UKIMWI (ATF)**

**Ndugu wananchi,** napenda pia kutumia maadhimisho haya kuhamasisha uchangiaji wa Mfuko wa Udhamini wa Kudhibiti UKIMWI (AIDS Trust Fund - ATF). Hivi karibuni nimeteua Bodi mpya ya Mfuko itakayotumika kwa kipindi cha miaka mitatu (2020 hadi 2023) baada ya Bodi ya awali kumaliza muda wake.

Nitumie nafasi hii kuwapongeza Wajumbe wa Bodi iliyopita kwa kazi nzuri waliyofanya na kuitakia mafanikio Bodi mpya. Bodi ya Mfuko iliyomaliza muda wake, katika kipindi cha **Julai 2016 hadi Juni 2019**, iliweza kukusanya jumla ya shilingi billioni **2.9 za kitanzania.**

Mgawanyo wa matumizi ya fedha za Mfuko kwa mujibu wa andiko lake ni: Asilimia sitini (60%) hutumika kununua dawa za ARV, dawa za magonjwa nyemelezi na vitendanishi; asilimia ishirini na tano (25%) hutumika kuimarisha huduma za kinga na asilimia kumi na tano (15%) hutumika kusaidia uwezeshaji na uratibu.

Fedha za Mfuko hupatikana kupitia fedha ambazo zinatolewa na Serikali na kupitishwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa

Tanzania; michango kutoka kwa wadau wa nje na wa ndani ya nchi na shughuli za uhamasishaji ikiwa ni pamoja na harambee.

**Ndugu Wananchi*,*** tangu kuanzishwa kwa Mfuko wa Udhamini wa Kudhibiti UKIMWI mwaka 2015, kumekuwa na mafanikio mbalimbali ikiwemo uwezo wa kununua dawa za magonjwa nyemelezi kwa Watu wanaoishi na VVU (WAVIU) kupitia Wizara ya Afya.

Mafanikio mengine ni kujengwa kwa Kituo cha kisasa kwa ajili ya kutolea huduma za VVU na UKIMWI kwa Watu wanaoishi na VVU eneo la Mirerani, Wilayani Simanjiro pamoja na kutoa huduma za kinga dhidi ya VVU kwa wakazi wanaozunguka Ziwa Victoria na visiwa vyake na kwa vijana wa vyuo vikuu na vya kati vilivyopo jijini Dodoma.

**Ndugu Wananchi,**

Natoa rai kwa wadau wa ndani na nje ya nchi, watoe michango yao kwa nia ya kutunisha mfuko huu kwa ajili ya kuokoa maisha ya Watanzania. Aidha, naiagiza Bodi mpya ya Mfuko kuendelea kusimamia na kuuendesha mfuko huu kwa uwazi na kuzingatia misingi ya utawala bora.

Hakikisheni kuwa unatumika kwa malengo yaliyokusudiwa. Wananchi wote pia mnakaribishwa kuchangia mfuko huu kwa kiwango chochote kupitia namba za simu **0684 90 90 90, ambayo ndani yake kuna 90 tatu za malengo ya kudhibiti UKIMWI.**

**MAELEKEZO MUHIMU**

Ili kuimarisha mikakati yetu na kakamilisha azma ya kufikia malengo ya Tanzania isiyokuwa na UKIMWI ifikapo 2030 ninatoa maagizo yafuatayo kwa Wizara ya afya na TACAIDS:

i. Kuendeleza mikakati ya kudhibiti maambukizi mapya ya virusi vya UKIMWI, ikwemo maambukizi ya mama kwenda kwa mtoto na Kifua Kikuu;
ii. Kuandaa mkakati endelevu wa kifedha kwa ajili ya kuimarisha Mfuko wa Udhamini wa Kudhibiti UKIMWI

Tanzania (AIDS Trust Fund - ATF) ili kuwahudumia vyema waathirika;

iii. Kuongeza programu zenye ubunifu zinazozingatia umri na jinsia zinazoshughulikia utambuzi wa hatari za maambukizo ya VVU na mikakati ya kupunguza madhara kwa kutumia nadharia sahihi za kubadili tabia;

iv. Kutumia uhamasishaji jamii wenye ufanisi ikiwemo redio za jamii kuibua uhitaji wa huduma za kinga, upimaji, matunzo na matibabu;

v. Kuhuisha na kujumuisha masuala ya UKIMWI(*mainstreaming*) kwenye taasisi na sekta zote ambazo zina mazingira yenye vichochezi vikuu vya UKIMWI, zikiwemo ujenzi, uchukuzi, uvuvi, madini; na

vi. Kuimarisha mfumo wa ufuatiliaji na tathmini wa huduma za UKIMWI nchini kote ili kuhakikisha huduma bora zinatolewa kwenye jamii.

**HITIMISHO**

**Ndugu Wananchi,** ninapoelekea kuhitimisha hotuba yangu napenda kuwajulisha kuwa Serikali inatambua mchango wa wadau mbalimbali ikiwemo nchi marafiki na sekta binafsi katika mapambano dhidi ya VVU na UKIMWI nchini. Nimefahamishwa kuwa leo nitatoa hundi ili kuziwezesha asasi za kiraia kutekeleza Afua mbalimbali za kipaumbele kwenye maeneo yao.

Hatua hiyo, imefanikishwa kwa kiwango kikubwa kupitia ushirikiano wa dhati uliopo kati ya kampuni ya *Geita Gold Mine* (GGM) na TACAIDS kwa njia ya harambee ya kupanda Mlima Kilimanjaro ijulikanayo kama ***Kili Challenge***. Nimejulishwa kuwa jumla ya Shilingi za Kitanzania Milioni 550 zitagawiwa kwa asasi hizo.

Huu ni mfano mzuri wa ushirikiano wa Serikali na sekta binafsi. Natoa wito kwa makampuni na wadau wa sekta binafsi kujitokeza kwa wingi na kuendelea kuunga mkono juhudi za Serikali.

**Ndugu wananchi*,*** kwa mara nyingine nawapongeza waratibu, waandaaji, wafadhili na watekelezaji wa kampeni zilizopita kama vile Furaha Yangu, ONGEA na Kipepeo ambazo zimeonesha

mafanikio makubwa. Nitoe rai kuwa kampeni hizi ziwe endelevu kwa sababu elimu bado inahitajika sana katika jamii ili kukumbushana kila wakati.

**Ndugu Wananchi,** nawapongeza sana wananchi wa Mkoa wa Kilimanjaro na Wadau wote kwa kufanikisha maadhimisho ya Siku ya UKIMWI Duniani mwaka huu. Nimefurahishwa na kiwango cha ufanisi wa maadhimisho haya. Hongereni sana. **"Mshikamano wa Kimataifa, Tuwajibike Kwa Pamoja".**

**Mungu Ibariki Afrika,**

**Mungu Ibariki Tanzania.**

**Asanteni sana Kwa kunisikiliza.**